Roho Mtakatifu

&

Miujiza

(The Holy Spirit

&

Miracles)

Na

Ellis P. Forsman

Roho Mtakatifu

&

Miujiza

Mambo ya kimwili hayaridhishi.

Mat. 4:4, "*Naye akajibu akasema, imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neon litokalo katika kinywa cha Mungu.*"

Yoh. 4:14, "*Walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.*"

Watu wengi wanakula, lakini bado wanabaki wakiwa na njaa

Je vyote ni vya asili?

BINADAMU ASIYE WA KAWAIDA

Zab. 19:1, "*Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake.*"

Rum. 1:10, "*Siku zote katika sala zangu nikiomba nije kwenu hivi karibu, Mungu akipenda kuifanikisha safari yangu.*"

Kuna wazo iliyopo nyuma ya asili

Roho hazionekani

Luka 24:39, "*Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.*"

1 Tim. 1:17, "*Sasa kwa mfalme wa milele asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina.*"

Mwanadamu ana roho isiyoonekana ndani na mwili unaoonekana nje.

Sehem ya mwanadamu kama Mungu (roho ya mwanadamu) haionekani nan i milele.

Roho hudhihirishwa

(zinafanywa zionekane)

2 Kor. 4:18, "*Tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.*"

1 Kor. 12:7, "*Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.*"

Je umeme siyo halisi, eti kwa sababu hauonekani?

Roho wa Mungu amefanya muonekano tofautitofauti

1 Kor. 12:4-6, "*Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye Yule. Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye Yule. Kasha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye Yule azitendaye kazi zote katika wote.*"

1 Kor. 12:11, "*Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.*"

Sababu tofauti zilihitaji utofauti

Kustaajabu kwa asili kumshuhudia Mungu

Mdo. 14:17, "*Lakini hakujiacha pasipo ushuhuda, kwa kuwa alitenda mema, akiwapeni mvua kutoka mbinguni na nyakati za mavuno, akiwashibisha miyo yenu chakula na furaha.*"

Heb. 3:4, "*Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu; ila yeye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu.*"

Muundo wa asili unamuonyesha muundaji

Maombi yaliyojibiwa ni msukumo wa Mungu wa asili.

Yak. 5:16-18, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii. Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe, na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita. Akaomba tena mbingu zikatoa mvua, nayo nchi ikazaa matunda yake.*"

Mungu anatawala na kuharibu asili

Mungu alitumia wingu kujibu maombi ya Eliya

Mungu angeweza kusababisha mvua pasipokuwa na mawingu (miujiza), lakini kwa hali isiyo ya kawaida ombi lililojibiwa linaweza lisiwe la miujiza

Mungu alianzisha vitu vyote kwa miujiza

Mwa. 1:1, "*Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu nan chi.*"

Mwa. 1:27, "*Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.*"

Nguvu ya Mungu ya ajabu inaonekana katika uumbaji wa miujiza

Lakini Mungu hakumuumba mwanadamu mwingine

Mwa. 1:28, "*Mungu akawabariki, Mungu akawaambia zaeni mkaongezeke, kaijaze nchi na kuitiisha ; mkatawale samaki wa baharini na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.*"

Ayu.10:18, "*Kwa nini basi kunitoa tumboni? Ningekata roho lisinione jicho lolote.*"

Mwanadamu aliyeumbwa kimiujiza hutokana na sharia za asili

Biblia iliiumbwa kwa uvuvio wa miujiza

2 Tim. 3:16, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

2 Pet. 1:21, "*Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya wanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.*"

2 Tim. 2:2, "*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.*"

Lakini hutolewa kwa mafundisho yasiyo ya kimiujiza

Mungu anaweza kuponya kwa kujibu maombi bila miujiza

Fil. 2:27, "*Kwa maana alikuwa hawezi kweli kweli, karibu na kufa; lakini Mungu alimhurumia; wala si yeye peke yake, ila na mimi pia; niwezi na huzuni juu ya huzuni.*"

Yak. 5:15, "*Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi atasamehewa.*"

Mungu anaharibu mfumo wa uponyaji wa mwili ili upone

Muujiza unakanganya sheria ya asili

Yoh. 3:2, "*Huyo alimjia usiku akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*"

Kut. 7:9, "*Farao atakaponena nanyi na kuwaambia, jifanyieni miujiza; ndipo utakapomwambia Haruni, shika fimbo yako, uibwage chini mbele ya Farao ili iwe nyoka.*"

Mtembea majini anaweza kutembea kwa kudhihirisha sheria ya asili, lakini Yesu alitembea majini kimiujiza

Yesu aliamuru dhoruba kukoma, na viashiria vya asili vikatii

Mat. 8:27, "*Wale watu wakamaka wakisema, huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zinamtii?*"

Mat. 9:8, "*Makutano walipomwona walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu aliyewapa watu amri ya namna hii.*"

Mashahidi walijua kwamba kitendo cha Mungu kinachozidi uwezo wa asili kimefanyika

Uzao wa mzazibu wa Mungu kubadilisha maji kuwa pombe kila kipindi inapokuwa

Yoh. 2:11, "*Mwanzo hbuo wa ishara Yesu aliufanya huko Kana ya Galilaya, akaudhihirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake wakamwamini.*"

Lakini Yesu aliizidi asili ili kuonyesha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu

Uzao wa bikra unachanganya aisili!

Kama hakuna nguvu izidiyo asili, sayansi inasema haiwezi ikatokea.

Luka 1:34, "*Mariamu akamwambia malaika, litakuwaje neon hili maana simjui mume?*"

Yoh. 1:14, "*Naye neon alifanyika mwili akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.*"

Tungeweza kutarajia uzao usio wa kawaida kama Yesu hakuwa mwanadamu wa kawaida

Yesu aliwafufua wale waliokufa kweli!

Lazaro alikuwa amekufa siku nne.

Yoh. 11:39, "*Yesu akasema liondoeni jiwe. Martha, dada yake yule aliyefariki akamwambia, Bwana ananuka sasa; maana amekuwa maiti siku nne.*"

Luka 8:53, "*Wakamcheka sana maana walijua ya kuwa amekwisha kufa.*"

Sheria ya asili haiwezi kumrudisha mtu aliyekufa kweli

Tukio la ghafla la miujiza ulikuwa ni mshangao, ajabu, na uoga

Marko 5:33, "*Na yule mwanamke akaingiwa na hofu na kutetemeka, akijua lililompata, akaja akamwangukia, akamweleza kweli yote.*"

Luka 7:16, "*Hofu ikawashika wote wakamtukuza Mungu, wakisema, Nabii mkuu ametoka kwetu; na Mungu amewaangalia watu wake.*"

Miujiza ilikuwa ni matendo mazuri ambayo ilipaswa kufanywa kwa uwezo wa Mungu tu

Miujiza ilionyesha kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu katika mwili wa mwanadamu

Yoh. 20:31, "*Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, sizizoandikwa katika kitabu hiki.*"

Kusudi lake ilikuwa ni kuonyesha ukuu wake – miujiza hueleweka tu pale ambapo kusudi lake linaeleweka

Miujiza pia ilionyesha huruma ya Mungu:

Kama Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu, angeonyesha huruma ya Mungu

Mat. 14:14, "*Walakini mitume Barnaba na Paulo, walipopata habari wakararua nguo zao, wakaenda mbio wakaingia katika makutano wakipiga kelele,*"

Heb. 4:15, "*Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.*"

Kutembea kwa Mungu miongoni mwa wanadamu wanaougu ingeweza kusemwa kama alivyokuwa Yesu

Dhumuni kuu la miujiza ilikuwa ni kuthibitisha na kuweka wazi neon la Mungu lililoandikwa na linalohubiriwa

Marko 16:20, "*Nao wale wakatoka wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neon kwa ishara zilizofuatana nalo.*"

Heb. 2:4, "*Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kaama alivyopenda mwenyewe.*"

Ukweli ukisha thibitishwa unakuwa umethibitishwa milele

Gal. 3:15, "*Ndugu zangu nanena kwa jinsi ya kibinadamu. Lijapokuwa ni agano la mwanadamu, hata hivyo likiisha kuthibitika, hakuna mtu alibatilishaye, wala kuliongeza neno.*"

Yoh. 20:29, "*Yesu akamwambia wewe kwa kuwa umeniona umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki.*"

Ninaamini kwamba Lincoln alikufa, ninaamini kuwa Yesu alikufa pia, pasipokuona yeyote kati yao akiidhinishwa

Miujiza ya Yesu iliandikwa chini ili kwamba wasomaji waelewe kweli kweli

Yoh. 20:31, "*Lakini hizi zimeaandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*

Efe. 3:3-5, "*Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. Kwa hayo myaasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho;*"

Miujiza ya Yesu iliandikwa katika maandiko, na muujiza wa uvuvio ukaaiandika

Biblia inasema wanadaamu hawataamini miujiza kama hawataamini maandiko yaliyo vuviwa.

Luka 16:31, "*Akamwambia, wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu.*"

Rum. 10: 17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Kama wanadamu wanatafuta mapenzi ya Mungu, "Imeandikwa", ila kama wanatafta hisia, watatafuta muujiza kwa hasara

Mitume wa Kristo waliongozwa katika "kweli yote"

(Hakuna ukweli zaidi utakaofunuliwa)

Kweli yote

Yoh. 16:13, "*Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote, kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*"

Yoh. 14: 25-26, "*Hayo ndiyo niliyowaambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu. Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia.*"

Ukweli wote uliofunuliwa toka kwa Mungu ilitolewa mara moja kupitia mitume ambao Yesu alifundisha.

Maandiko yote yamevuviwa na Mungu imekamilika katika kila tendo jema

2 Pet. 1:3, "*Kwa kuwa uweza wwake na Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kujua yeye aliyetuita kwa utukufu, ...*"

2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

kama kwa maandiko kazi yetu inaweza kukamilika, ni nini zaidi au ni nini zaidi tunachohitaji?

Roho Mtakatifu alitolewa kwa njia tofauti ili makusudi tofauti iweze kutimizwa.

1 Kor. 12:4-6, "*Basi pana tofauti za karama; baali Roho ni yeye yule. Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule. Kasha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika yote.*"

Kila udhihirisho katika maandiko hautokei kwangu leo

Kwa sababu tu udhihirisho wa Roho wa Mungu ulitolewa kwa kusudi maalum haimanishi kwamba nimehaidiwa leo.

Yohana 1:32, "*Tena Yohana akashuhudia akisema, nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake.*"

Hii hapa ahadi ya Roho – je imetokea kwako leo?

"Njiwa wangu yuko wapi?" Ninaweza kuuliza, "Ilihaidiwa katika maandiko na Mungu"

ALIHAIDIWA! ***Sio kwangu!***

ALITOLEWA! ***Siyo kwa ajili yangu!***

WANGU? ***Kwa Yohana pekee!***

Yohana 1:33-34, "*Wala mimi sikumjua; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu.*"

Kila ahadi iliyotokea ilikuwa na kusudi, na kusudi halipo leo

Mwili wa Yesu ulitolewa naa Roho Mtakatifu, vipi kuhusu wako?

Umetolewa na Roho Mtakatifu

Mat. 1:20, "*Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto akisema, Yusufu mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.*"

Kwa sababu tu iko kwenye Biblia haimanishi kwamba ilinitokea.

Yesu anahusika na Roho katika Utatu Mtakatifu, je wewe?

Baba **Mwana**

Utatu Mtakatifu

Roho Mtakatifu

Kol. 2:9, "*Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya kimwili.*"

Mat. 28: 19, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;*"

Kuhusu Roho ipo ndani ya Biblia, lakini haimanishi mimi hata kidogo

Yesu alipokea ahadi ya kumtuma Roho kutoka mbinguni, lakini mimi siwezi!

KRISTO

MITUME

Mdo. 2:33, "*Basi yeye akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia.*"

Je nitarajie kupokea ahadi kwa sababu ipo ndaani ya Biblia?

Kusudi tofauti ilihitaji udhihirisho tofauti

(Kwa Yesu) **Utatu Mtakatifu**	**(Kwa Mitume wake)** **Haieleweki**
(Kwa Manabii waliovuviwa) **Uvuvio**	**(KwaWakristo wote)** **Kujawa**

Jinsi Roho Mtakatifu alivyotolewa

(Kwa Yesu) **Mwili wake ulikuwa na manyoya ulishuka kama njiwa pamoja katika utatu Mtakatifu Roho iliyotumwa toka mbinguni**	**(Kwa mitume wake)** **Ndimi zenye moto vichwani ikivuma kama upepo wakinena lughaa wasizojifunza wakitiwa nguvu na Roho**
(Kwa manabii waliovuviwa) **Kwa kuwekewa mikono ya mitume uvuvio wa miujiza** **Karama tisa au nguvu ili kufunua, na kulithibitisha neno**	**(Kwa Wakristo wote)** **Kujawa karama, uwepo wa Mungu, nguvu ya Mungu katika hema lake, hakuna miujiza**

Ukitumia kwa halali Neno la Kweli inaahitaji matumizi sahihi ya karama

Kuhusu YESU **kuhusu MANABII**

Kwa WAKRISTO WOTE

Kwa ajili

Ya MITUME

2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

2 Pet. 3:16, "*Vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe.*"

Ninaweza kuyapindisha maandiko kwa uharibifu wangu mwenyewe

Je wote ni Mitume?

Je wote ni manabii?

Mtume Nabii Mkristo

1 Kor. 12:28-29, "*Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina ya lugha. Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza?*"

Usidai ahadi waliopewa mitume isipokuwa wewe ni Mtume

Je Wakristo leo wanaweza kuonyesha ishara ya Mtume?

"ISHARA" NI NENO MOJA LINALOMANISHA "MUUJIZA"

2 Kor. 12:12, "*Kweli ishara za mtume zilitendwa katikati yenu katika saburi yote, kwa ishara na maajabu na miujiza.*"

Je unaweza kufanya miujiza kama ya Mtume?

Kuwafufua wafu ilikuwa ni moja ya miujiza ya Mitume

Mat. 10:2, 5, 8, "*Na majina ya hao mitume kumi na wawili ni haya; wa kwanza Simoni aliyeitwa Petro, na Andrea nduguye; Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye; ... Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza akisema katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure.*"

Petro alifanya! Mdo.9:40, "*Petro akawatoa nje wote, akapiga magoti akaomba, kasha akaelekea yule maiti akanena, Tabitha ondoka naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro akajiinua akaketi.*"

Paulo alifanya! Mdo. 20:9-10, "*Kijana mmoja jina lake Eutiko dirishani, akalemewa na usingizi sana; hata Paulo alipoendelea sana kuhubiri, akazidiwa na usingizi wake akaanguka toka orofa ya tatu; akainuliwa amekwisha kufa. Paulo akashuka akamwangukia, akamkumbatia, akasema msifanye ghasia maana uzima wake ungalimo ndani yake.*"

Kutoa pepo ilikuwa moja ya ishara (miujiza) ya Mitume

Marko 16:17-18, "*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*"

Mat. 10:1, "*Akawaita wanafunzi wake <u>kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe</u>, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina.*"

Mat. 10:5, 8, "*<u>Hao Thenashara</u> Yesu aliwatuma, akawaagiza akisema, katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, <u>toeni pepo</u>;...*"

Ni mitume pekee ndio walikuwa na uwezo wa kutoa pepo

Kwa nini wengine wanadai kuwa na ahadi za mitume, lakini hawatii maagizo zilizoambatana nazo?

Mat. 10:5, 9-10, "*Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza akisema, katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie. Msichukue dhahabu, wala fedha, wala mapesa mishipini mwenu; wala mkoba wa safari, wala kanzu mbili, wala viatu, wala fimbo; maana mtenda kazi astahili posho lake.*"

Wanadamu leo wanachukua dhahabu, koti 2, viatu, na kwenda kwa mataifa

Tumia kwa halali maagizo kwa mitume kutoka katika maagizo ya Wakristo

Yesu alihaidi nguvu ya kimitume kwa Mitume wake, alafu wakayathibitisha kwa maneno yao kwa ishara zilizofuata!

Mitume kumi na moja Hawakuamini ms. 14	Ishara zilizofuata baada ya kuamini **Mitume** Ms. 17-18	Bwana alitendaa ishara pamoja na **Mitume** Ms. 20.

Marko 16:14, "*Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.*"

Marko 16: 17, "*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya.*"

Marko 16: 20, "*Nao wale wakatoka wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo*."

Siyo wakristo wote katika ulimwengu wote walihaidiwa nguvu hizi!

Mitume kumi na wawili, siyo wale wengine 120, walipokea nguvu ya umitume siku ya Pentekoste

Mdo. 1:5, "*Ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.*"

Mdo. 1:8, "*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashihidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*"

Ninyi ambao? Mdo. 1:2, "*Hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua;*"

"Wale" ambao Yesu aliahidi nguvu ya kimitume walikuwa <u>Mitume.</u>

Uthibitisho unaoonyesha kwamba nguvu ya miujiza ilikuja juu ya Mitume siku ya Pentekoste

Mdo. 1:8, "*Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wan chi.*" "*Enyi*" inamanisha watu wa Galilaya" (Mdo 1:11, "*... Enyi watu wa Galilaya…*")

Mdo. 2:1, "*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja.*" Mdo. 1:26, "*…Wakawapigia kura, kura ikamwangukia Mathiya; naye akahesabiwa kuwa pamoja na mitume kumi na mmoja.*"

Mdo. 2:7, "*.. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, tazama hawa wote wasemao si Wagalilaya?* Mdo. 2:13-14, "*Wengine walidhihaki wakisema, wamelewa kwa mvinyo mpya. Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti akawaambia, enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili mkasikilize maneno yangu.*"

Mdo. 2:37, "*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu?*"

Mitume walijaa katika Roho wa Mungu siku ya Pentekoste

Petro alisema kuw Kornelio alipokea zawadi inayofanana na ile waliopokea Mitume hapo mwanzo!

Mdo. 10:46, "*Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu…*"

Mdo. 11:15, "*Ikawa nilipoanza kunena Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo.*"

Mdo. 11:17, "*Basi ikiwa mwenyezi Mungu amewapa karama ile ile aliyotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu?*"

Mungu alikuwa na kusudi maalum kwa zawadi hii juu ya familia ya mataifa

Tuyaache maandiko yaelezee kusudi ya Kornelio kupata nguvu yaa moja kwa moja badala ya kuhitimisha kwamba wote wanapaswa kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Kwa nini alitiwa nguvu hivyo?

Hakuwa Myahudi (Mtaifa). Mdo. 10:28, 35, 45, "*Akawaambia, ninhyi mnajua ya kuwa si halali mtu asiye Myahudi ashikamane na mtu aliye wa taifa linguine wala kumwendea, lakini Mungu amenionya nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi. …Bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa nay eye. …Na wale waliotahiriwa, walioamini wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Petro alisema kwamba Mungu hana upendeleo kwa mwanadamu. Mdo. 10:34-35, "*Petro akafumbua kinywa chake, akasema, hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye.*"

Wayahudi walistajabu kwamba Roho Mtakatifu amewaijia Mataifa. Mdo. 10: 45, "*Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Petro alishawishika kuwabatiza. Mdo.10:47, "*Ni nani awazaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama na sisi?*"

Karama kama hizi zilidhihirisha kwamba Mataifa walihakikishiwa toba liletalo uzima. Mdo. 11: 17-18, "*Basi ikiwa Mwenyezi Mungu amewapa wao karama ile ile aliyotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu? Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu wakisema, basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*"

Petro alieleza kwamba kuonekana kwa Roho Mtakatifu katika mfumo huu ulikuwa ni ushahidi wa Mungu kuwakubali Mataifa. Mdo. 15:7-9, "*Na baada ya hoja nyingi Petro akasimama akawaambia ndugu zangu ninyi mnajua ya kuwa tangu siku ya kwanza Mungu alichagua miongoni mwenu ya kwamba mataifa wasikie neno la injili kwa kinywa change na kuliamini. Na Mungu ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia akiwapa Roho Mtakatifu vile vile kama alivyotupa sisi;*"

Ukweli wa mataifa kukubaliwa ulithibitishwa mara moja na haikuwahi kuthibitishwa tena

Yesu alifanya ahadi ya kipekee ya nguvu kwa Mitume wake ambao wangeleta ulimwenguni neno la kweli lililo kamilika

Mdo. 1:8, "*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wan chi.*"

Yohana 15:26, "*Lakini ajapo huyo msaidizi, nitakaye wapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba yeye atanishuhudia.*"

Yohana 16:13, "*Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hata nena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*"

Mat. 18:18, "*Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani, yatakuwa yamefungwa mbinguni, na yo yote mtakayoyafungua duniani, yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*"

1 Kor. 12:28-29, "*Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kasha miujiza, kasha karama za kuponya wagonjwa na masaidiano na maongozi na aina za lugha. Je wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza?*"

Nilifungalo duniani litakuwa limefungwa mbinguni!

"Kweli yote ilikuja kupitia mitume na wale waliowekewa mikono na mitume

Yohana 16:13, "*Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*"

Mat. 18:18, "*Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani, yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*"

Mtume na wale waliowekewa mikono waliandika vitabu vyote vya Agano Jipya.

Baadhi ya kweli ilikuja kupitia kuwekewa mikono na Mitume

Efe. 3:5, "*Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho.*"

1 Kor. 12:28, "*Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kasha miujiza, kasha kaarama zaa kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.*"

Efe. 4:11, "*Naye alitoa wengine kuwa mitume na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu.*"

Mitume waliwapa nguvu ya uvuvio ya kunena na kuandikwa

Ni Mitume pekee nido waliotoa nguvu ya uvuvio kwa kuwawekea mikono

Mitume walitoka Samaria ili kufaanya kile ambacho Filipo, mwinjilist asingeweza kufanya.

Mdo. 8:14-18, "*Na mitume waliokuwako Yerusalemu waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikoni yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha*."

2 Tim. 1:6, "*Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu.*"

Mdo. 19:6, "*Na Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri.*"

Uvuvio ulikuja kupitia mitume

Mpangilio wa Mungu wa kazi uliruhusu uvuvio kukoma wakati mitume na manabii walipofariki wote

Yuda 1:3, "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*"

1 Kor. 15:8, "*Na mwisho wa watu wote alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake.*"

Ufu. 22:18-19, "*Namshuhudia kiala mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.*"

Uvuvio ulikoma kwa Mitume na manabii

Baadhi ya mafundisho ya Agano Jipya ni lazima zitumiwe kwa halali ili ziendane na mitume waliovuviwa na manabii na sio kwetu LEO!

Mat. 10:19-20, "*Lakini hapo watakapowapeleka , msifikri –fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.*"

Leo hii tumepewa tunachokinena: imeandikwa kikamilifu katika maandiko

1 Kor. Sura za 12-14 ni maagizo kwa watu waliovuviwa maandiko yalipokuwa hayajakamilishwa

Wamarekani hawafuati sheria iliyopo ya muda mfupi katika kifungu cha shirikisho, kwa vile sasa tupo chini ya katiba ya Marekani na sasa hatupo chini ya vifungu hivi.

Tunajifunza ili kutumia kwa halali

Yesu alitoa karama za miujiza… HADI KUFIKIA UMOJA WA IMANI”

Efe. 4:7-8, 11, 13, “*LAkini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. Hivyo husema, alipopaa juu aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa. Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwaa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu. Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, na kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo;*”

“Umoja wa Imani” ilikuwa ni imani kama umoja (imefunuliwa kabisa)

1 Kor. 13:9-10, “*Kwa maana tunafahamu kwa sehemu, na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile kamili iliyo kwa sehemu itabatilika.*”

Hatutarajii “sehemu” zaidi (ufunuo wa miujiza) ili kuongezwa katika ufunuo wa Mungu uliokamilika

Ufunuo ambao haukukamilika ulitoa nafasi kwa maandiko yaliyokamilika

Ni kama mwandishi anavyoweza kuandika kurasa na sura tofauti, alafu anaziweka vyote pamoja ili kuunda kitabu kilicho kamilika, hivyo sehemu kwa sehemu karama ya muda mfupi ya uvuvio sasa ni mbadala wa ufunuo uliokamilika.

Efe. 3:4, “*Kwa hayo myasomapo mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo.*”

Ufunuo wa Mungu uliokamilika umekuja

Karama za miujiza ya unabii, ndimi, na ujuzi ulifunuliwa, ilitengenezwa na ikapangwa kukoma

1 Kor. 13:8, "*Upendo haupungui neno wakati wowote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha zitakoma; yakiwapo maarifa yatabatilika.*"

(Karama za miujiza ya ujuzi na unabii) 1 Kor. 13:2, "*Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo si kitu mimi.*"

Biblia hiyo iyo inayosema ufunuo wa miujiza ilitokea, ndiyo inayosema zilikoma

Ufunuo wa Mungu uliokamilika katika maandiko ni "bora" kuliko karama ya miujiza ya muda mfupi nay a sehemu kwa sehemu

1 Kor. 12:31, "*Takeni sana karama zilizo kuu. Hataivyo nawaonyesha njia iliyo bora.*"

1 Kor. 13:12, "*Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana.*"

Ufunuo uliokamilika ni bora kuliko vijisehemu, na ile ya muda mrefu ni bora kuliko ile ya muda mfupi!

Maneno yenye nguvu nay a wazi hutumika katika kuelezea wakati karama ya miujiza ya wakati fulani.

1 Kor. 13:8, "*Upendo haupungui neno wakati wowote; bali ukiwapo unabii utabatilikaa; zikiwapo lugha zitakoma; yakiwapo maarifaa yatabatilika.*"

1 Kor. 13:10, "*Lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika.*"

Ni maneno yapi yenye nguvu ambayo ingetumiwa kusema kwamba nguvu ya miujiza ya uvuvio ingekoma?

Paulo anafananisha ufunuo wa muda mfupi ambao ni wa sehemu kwa sehemu na kioo chenye giza kulinganisha na maandiko yaliyokamilika

Yakobo 1 :22-24, "*Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kasha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.*"

Maandiko yanamuonyesha mwanadamu jinsi alivyo – uso kwa uso

Imani, tumaini na upendo zitakaa kama unabii, ndi

mi, na ujuzi wa miujiza ukikoma kwa kuja kile ambacho ni kamilifu

"*Ile iliyokamili*" haimanishi kuja kwake Kristo mara ya pili au mbingu kwa sababu kwa wakati huo imani na tumaini hazitaendelea.

Rom. 8: 24-25, "*Kwa maana tulikolewa kwa taraja; lakini kitu kilichotarajiwa kikionekana , hakuna taraja tena. Kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho? Bali tukikitarajia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi.*"

Heb. 11:1, "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*"

Imani na Tumaini vilikuwepo wakati wa ukamilisho wa maandiko.

Kwa vile ujumbe wa Roho Mtakatifu umekamilika na kuhitimishwa katika maandiko, haneni kwa njia nyingine yoyote

2 Tim. 3:17, "*Ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

2 Yohana 1:9, "*Kila apitayhe cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*"

Hakuna nyongeza katika maandiko inayohitajika au inayoruhusiwa leo.

"Ufunuo" unaodaiwa kuwepo leo unatofautiana na "ujumbe" unaofunuliwa, lakini Mungu siyo wa machafuko

1 Kor. 14:33, "*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vilevile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.*"

Rum. 16:17, "*Ndugu zangu nawasihi waangalieni wale wafanyuao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliojifunza; mkajiepushe nao.*"

Ufunuo wa Roho Mtakatifu mar azote ilifundisha kitu kilekile, lakini "ufunuo" wa leo unatofautiana na Biblia na kila mmoja

Wakristo wanamsikiliza Roho Mtakatifu wanaposikiliza neno la Mungu

Heb. 3:7, "*Kwa hiyo kama anenavyo Roho Mtakatifu, leo kama mtaisikia sauti yake.*"

Ufu. 2:11, "*Yeye aliye na sikio na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.*"

Roho ananena katika maandiko tu!

Tunamsikiliza kwa kusikiliza ujumbe wake!

Maandiko siyo maneno ya binadamu au ujumhe, bali ya Roho Mtakatifu

1 Kor. 2:13, "*Nayo twayanena si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.*"

1 Thes. 2:13, "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mliilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.*"

Gal. 1:12, "*Kwa kuwa sikuipokea kwa wanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.*"

Maandiko ni maneno ya Roho Mtakatifu

Chochote anachofanya Roho Mtakatifu kwa <u>ujumbe</u>, anafanya hivyo kupitia Biblia, kwa vile Biblia ndiyo <u>ujumbe wake uliokamilika</u>!

Kinachosemwa kuja kufanywa	**Mistari isemayo ilifanywa na Roho Mtakatifu**	**Mistari isemayo ilifanywa kwa Neno**
Walichomwa	**Yohana 16:7-8**	**Mdo. 2:37**
Kuokolewa	**Yohana 3:5**	**Yakobo 1:21**
Kuzaliwa	**Yohana 3:5**	**1 Pet. 1:23**
Kuoshwa	**1 Kor. 6:11**	**Efe. 5:26**
Takaswa	**1 Kor. 6:11**	**Yohana 17:17**
Kudhihirishwa	**1 Kor. 6:11**	**Rum. 5:1; 10:17**
Kuokolewa	**Tito 3:5**	**Yakobo 1:21**

Roho Mtakatifu anafanya vitu hivi kupitia neno!

Mti hukatwa na <u>mtu</u>, lakini pia hukatwa na <u>shoka</u>. Inakatwa na mtu kwa <u>kutumia</u> shoka.

Efe. 6:17, "*Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu;*"

Heb. 4:12, "*Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena la choma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*"

Roho wa Mungu hukata nafsi ya mwanadamu kupitia neno!

<u>Ufunuo</u> wa Roho, siyo <u>tendo</u> lake ambalo lingekoma. Hataivyo uvuvio wa ujumbe wake umekamilika, ila <u>matendo</u> yake hayajakamilika!

Fil. 2:13, "*Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.*"

Efe. 3:16, "*Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*"

Roho Mtakatifu wa Mungu ni uwepo wake na nguvu ndani ya Wakristo

<u>Ujumbe</u> wa Roho unapatikana katika Biblia tu, lakini <u>matendo</u> yake hayapo katika Biblia tu

Efe. 3:16, "*Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*"

Efe. 3:20, "*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;*"

Mwanadamu anahitaji <u>uwepo</u> wa Mungu na <u>nguvu</u> pamoja na ujumbe wake uliokamilika

Ambacho Mungu “amekamilisha” katika Biblia ni ujumbe wa wokovu, lakini tunahitaji msaada wake pia na ushirika

2 Tim. 3:15-17, “*Na kwa kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika hali; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*”

Watoto wanahitaji msaada pamoja na ujumbe toka kwa wazazi wao

Watoto wana Roho wa Mungu ndani yao kama zawadi toka kwa Mungu

Mdo. 2:38-39, “*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*”

Mdo. 2:41, “*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*”

Ni zawadi gani kubwa ambayo Mungu angeweza kutoa isipokuwa nguvu yake na uwepo wake kukaa ndani yetu?

Karama ya kuwa na Roho siyo miujiza, siyo uvuvio, siyo hisia – isipokuwa ni Mungu yu miongoni mwa watoto wake

Mdo. 5:32, “*Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio.*”

Rum. 5:5, “*Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.*”

1 Thes. 4:8, “*Basi yeye anayekataa, hakatai mwanadamu bali Mungu anayewapa ninyi Roho wake Mtakatifu.*”

1 Yoh 3:24, “*Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.*”

1 Yoh. 4:13, “*Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametushirikisha Roho wake.*”

Gal. 4:6, “*Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu aliaye, Aba, yaani Baba.*”

Yak. 4:5, “*Au wadhani ya kwamba maandiko yasema bure? Huyo Roho akaaye ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu.*”

2 Tim. 1:14, "*Ilinde ili amana nzuri kwa Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu.*"

Rum. 8:9, "*Lakini ikiwa Roho Mtakatifu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.*"

Rum. 8:11, "*Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yetu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.*"

Fil. 1:19, "*Maana najua ya kuwa haya yatanigeukiwa kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya kuomba kwenu na kuruzukiwa Roho wa Yesu Kristo.*"

Mistari hii inaelezea "zawadi" na "kukaa"

Roho wa Mungu anakaa kwenye mwili wa Mkristo kama hekalu

1 Kor. 3:16, "*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, nay a kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?*"

1 Kor. 6:19, "*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe;*"

Efe. 2:22, "*Katika yeye ninyi nanyi mmejengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*"

Mdo. 17:24, "*Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye kwa kuwa ni Bwana wa mbingu nan chi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono.*"

Mdo. 17:28, "*Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu mtunga mashairi alivyosema, maana sisi sote tu wazao wake.*"

Hekalu ni mahali panapokaa utukufu

Kwa Roho tunaziuwa matendo ya mwili

Gal. 5:16-17, "*Basi nasema enendeni kwa Roho wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka.*

Rum. 8:13, "*Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.*"

Efe. 3:16, "*Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*"

Nguvu ya Roho hubadilisha vita binafsi katika miili yetu kuwa ushindi

Aliyeko ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye duniani

1 Yoh. 4:4, "*Ninyi watoto wadogo mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.*"

Yuda 1:19, "*Watu hao ndio waletao matengano, watu wa dunia hii tu, wasio na Roho.*"

Rum. 8:26, "*KAdhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.*"

Efe. 5:18, "*Tena msilewe kwa mvinyo ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho;*"

Fil. 2:13, "*Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.*"

Kwa vile shetani hujaribu na kuwadhoofisha Wakristo kwa mafundisho ya uongo na ubinafsi, Roho Mtakatifu humtia nguvu mtu binafsi.

Nguvu ya Mungu hufanya kazi ndani ya Wakristo!

Efe. 3:20, "*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.*"

Efe. 3:16, "*Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*"

1 Kor. 6:19-20, "*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzenu Mungu katika miili yenu.*"

Efe. 1:13, "*Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu; tena mmekwisha kumwamini yeye na kutiwa mhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.*"

Rum. 8:11, "*Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yetu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.*"

Roho ndiye chanzo cha nguvu zetu

Gal. 5:16, "*Basi nasema enendeni kwa Roho wala hamtazitimiza kamwe tama za mwili.*"

Gal. 5:22, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*"

Gal. 5:25, "*Tukiishi kwa Roho na tuenende kwa Roho.*"

Efe. 5:18, "*Tena msilewe kwa mvinyo ambapo mna ufisadi; bali mjazwe Roho;*"

Rum. 8:14, "*Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.*"

Rum. 8:26-27, "*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.*"

Efe. 6:18, "*Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatufu wote.*"

Fil. 2:1, "*Basi ikiwako faraja yo yote katika Kristo, yakiwako matulizo yoyote ya mapenzi, ukiwako ushirika wowote wa Roho, ikiwako huruma yoyote na rehema,*"

2 Kor. 13:14, "*Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho mtakatifu ukae nanyi nyote.*"

Shetani anafanya miujiza ya uongo!

2 Thes. 2:9, "*Maana ndugu mnakumbuka taabu yetu na masumbufu yetu; kwa kuwa mchana na usiku tulifanya kazi tusije tukamlemea mtu wa kwenu awaye yote, tukawahubiri hivi injili yaa Mungu.*"

Ufu. 13:13, "*Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu.*"

Mat. 7:22, "*Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?*"

2 Kor. 11:13-15, "*Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao*."

Kumb. 13:1-3, "*Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto akikutolea ishara au ajabu, itakuwa hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, na tuifuate miungu mingine usiyoijua na tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa BWANA Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote.*"

2 Thes. 2:10-11, "*Na katika madaanganyo yote na udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli wapate kuokolewa. Kwaiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu wauamini uongo.*"

2 Yoh. 1:10-11, "*Mtu akija kwenu naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye salamu azishiriki kazi zake mbovu.*"

Thibitisha kila mwalimu kwa maandiko!

1 Thes. 5:21-22, "*jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema; jitengeni na ubaya wa kila namna.*"

1 Yoh. 4:1, "*Wapenzi msiamini kila roho bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu, kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani*."

1 yoh. 4:6, "*Sisi twatokana na Mungu. Yeye amjuaye Mungu atusikia; yeye asiyetokana na Mungu hatusikii. Katika hili twamjua Roho wa kweli, na roho wa upotevu.*"

Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"

Kama haiwezi kuthibitishwa na maandiko kuwa ni cha kweli, basi haiwezi kuwa kweli!

Ndimi za kisasa hushindwa jaribio la Bwana!

Mdo. 2:6, "*Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe.*"

Mdo. 2:8, "*Imekuaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliozaliwa nayo?*"

1 Kor. 14:1, "Ufuateni upendo na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu.

1 Kor. 14:19, "*Lakini katika kanisa napenda kunena maneno matano kwa akili zangu nipate kuwafundisha wengine, zaidi ya kunena maneno kumi elfu kwa lugha*."

1 Kor. 14:22, "*Basi hizi lugha ni ishara, si kwao waaminio, bali kwao wasioamini lakini kuhutubu si kwa ajili yao waaminio.*"

1 Kor. 14:27-28, "*Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu na mmoja afasiri. Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu.*"

1 Kor. 14:33-34, "*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote yaa watakatifu. Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena bali watii, kama vile inenavyo torati nayo.*"